

Utangulizi

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ni Wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto yenye jukumu la kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendantishi.

Pamoja na kazi zingine zinazofanywa na Mamlaka katika kulinda Afya ya Jamii, TMDA hudhibiti matangazo ya biashara kwa kuyatathmini na kutoa vibali kabla ya kuyaruhusu ili kujihakikishia kwamba taarifa zilizomo hazipotoshi umma.

Ni matangazo ya bidhaa zipi yanayodhibitiwa na TMDA?

TMDA inadhibiti matangazo ya biashara ya bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendantishi.

Nini lengo kuu la kudhibiti matangazo hayo?

Kwa kawaida mfanyabiashara hutumia tangazo kufanya bidhaa yake ijulikane na vilevile kuwashawishi watumiaji kutumia bidhaa hiyo.

Kutokana na hali hiyo, TMDA ina jukumu la kusimamia na kuhakikisha kuwa matangazo yanayohusiana na dawa, vifaa tiba na ya vitendantishi hayana taarifa za upotoshaji.

Aidha, mlaji, msikilizaji mtazamaji, msomaji anatakiwa kuwa mwangalifu na maneno ya kibiashara yanayotumiwa na watengenezaji na wauzaji katika matangazo mfano baadhi ya matangazo kama vile "dawa fulani inatibu UKIMWI", "dawa hii inatibu magonjwa mengi na haraka" au "dawa hii haina madhara ye yote kwa mtoto au mkubwa". Bidhaa zeny sifa za namna hii hazipo. Hivyo ni jukumu la Mamlaka kuhakikisha inazuia upotoshaji wa aina hii katika matangazo

Je, ni hayo tu yanayosababisha kudhibiti matangazo ya dawa, vifaa tiba na vitendantishi au kuna umuhimu gani zaidi?

Ni muhimu kudhibiti matangazo kwani watu au walaji wengi hawafahamu kwa undani kuhusu bidhaa hizi hivyo basi kuweza kuamini kila kitu muuzaji au mtengenezaji anachosema au kilichoelezwa katika bidhaa husika.

Maelezo ya bidhaa yenye kupotosha yanaweza kumfanya mlaji kutumia pesa nyingi bila ya kupata au kufaidika na kile muuzaji au mtengenezaji alichosema au kutangaza.

Mfano wa bidhaa kama dawa, undani au ukweli au taarifa sahihi kuhusu dawa sio watu wengi wanaweza kufahamu, kwani fani hii ni ya kitaalam na ni wachache tu walijonayo. Hivyo basi udhibiti wa matangazo unasaidia kuzuia matangazo yenye taarifa potofu na kuweka suala la biashara mbele yasifike kwa wananchi.

Ni vigumu kwa mlaji wa kawaida kufahamu au kuthibitisha kuwa maelezo katika tangazo la biashara ni ya kweli au laa. Hivyo kinahitajika chombo cha kutoa maelezo au kulinda maslahi ya mlaji asipotoshwe katika kufanya maamuzi yake wakati wa kununua bidhaa na kupoteza pesa zake pasipo sababu za msingi au kwa udanganyifu fulani.

Ni matangazo yapi au ya namna gani TMDA ina jukumu la kuyadhibiti?

Matangazo yanayodhibitiwa na TMDA yamegawanyika katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni yale yanayowalenga wataalam wa Afya na kundi la pili ni yale yanayomlenga moja kwa moja mtumiaji au mlaji.

Matangazo haya kwa ujumla huwafikia walengwa kupidia vipeperushi, vijarida, mikutano, semina, warsha, maonesho, kudhamini kongamano na kutoa sampuli za bidhaa bure hususan kwa wataalam wa afya. Pia matangazo huwafikia walengwa kwa njia ya redio, runinga, mabango na mitandao ya kijamii na udhamini wa michezo au vipindi mbalimbali kwenye radio au runinga na kwenye vifungashio vyta bidhaa husika.

Ni utaratibu gani unaotumika katika kudhibiti matangazo hayo?

Mtangazaji wa dawa, vifaa tiba na vitendantishi anatakiwa kupata kibali au ruhusa ya kimaandishi ya kutangaza bidhaa yake kutoka TMDA, kabla ya kurusha au kutoa tangazo lake.

Mtangazaji wa bidhaa anatakiwa kuleta tangazo lake ofisi za TMDA, likiwa katika hali ya kimaandishi (script) na hali yake halisi ya utangazaji, yaani kama litawekwa kwenye runinga basi liletwe katika hali au mfumo huo.

Tangazo hilo litatathminiwa kuona kama limekidhi matakwa ya Mwongozo wa Udhibiti wa Matangazo ya Bidhaa na halina upotoshaji.

Aidha, matangazo yasiyokidhi viwango viliviyowekwa, mhusika huagizwa kutayarisha tangazo lingine linalokubalika kabla ya kupewa kibali au ruhusa kimaandishi ya kutangaza bidhaa husika kwa umma.

Wananchi wanashirikishwaje na anaweza kusaidia vipi Mamlaka katika utaratibu au zoezi hili la udhibiti wa matangazo kwa ujumla?

Mwananchi au mlaji ana mchango mkubwa sana kwa Mamlaka katika shughuli hii ya udhibiti wa matangazo ya dawa, vifaa tiba na vitendashi.

Shughuli ya udhibiti wa matangazo ya bidhaa hizi inategemea sana mlaji au mwananchi kwani sasa hivi kumekuwa na vyombo vingi vya habari na mitandao ya kijamii vilivyopo katika maeneo mbalimbali nchini. Hivyo inakuwa vigumu kwa TMDA pekee kufanya ufuutiliaji wa matangazo yote yanayotolewa. Mlaji anatakiwa kutoa taarifa kwa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba pale anapoona, kuhisi au kusikia tangazo ambalo anadhani lina upotoshaji ndani yake kwa bidhaa zinazodhibitiwa na Mamlaka.

Pia ifahamike kuwa taarifa ya mlaji atakayotoa kwa Mamlaka itafanywa kuwa siri na kumlinda aliyetua taarifa hiyo. Mto taarifa anatakiwa kutoa taarifa kuwa ni lini na muda gani tangazo hilo ameliona au kulisikia kutoka kwenye chombo gani cha habari au katika nyenzo yejote ya kutangazia.

USHAURI:

Mamlaka inapenda kushauri wananchi wote kwa ujumla kwamba, pale wanapoona au kusikia tangazo la biashara la dawa, vifaa tiba na vitendanishi ambalo mtumiaji analitilia shaka kwamba taarifa zake hazina ukweli au zimelenga kupotosha umma basi asisite kutoa taarifa kwa Mamlaka ili tangazo hilo liweze kushughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi unaotakiwa mapema.

Tunapenda vile vile kutoa wito kwa vyombo vya habari kutokutoa matangazo ya kibiashara ya dawa, vifaa tiba au vitendanishi ambayo hayana kibali kutoka TMDA.

Kama una swali au maoni tuandikie kuitia:

Mkurugenzi Mkuu,

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA),

S.L.P 1253 Dodoma au 77150 Dar es salaam.

Simu+255 22 2450512/2450751/2452108

Barua pepe: info@tmda.go.tz

Tovuti: www.tmda.go.tz

Simu bila malipo: 0800110084



Unaweza pia kuwasiliana nasi kuitia katika Ofisi zetu za Kanda.

Kanda ya Ziwa

Barabara ya Nyasaka,

Nyakato Buzuruga,

S.L.P 543,

Ilemela - Mwanza

Simu +255 28 2981224/5

Barua pepe: info.mwanza@tmda.go.tz

Kanda ya Kaskazini

Eneo la Sakina.

S.L.P 16609, Arusha

Simu +255 272970333/737782442

Barua pepe: info.arusha@tmda.go.tz

Kanda ya Mashariki

Jengo la GEPF,

Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,

S.L.P 31356,

Dar es salaam,

Simu +255 739 226328/788470312

Barua pepe: info.easternzone@tmda.go.tz

Kanda ya Nyanda za Juu Kusini

Jengo NHIF ghorofa ya 3.

S.L.P 6171, Mbeya

Simu +255 252504425

Barua pepe: info.mbeya@tmda.go.tz

Kanda ya Kati

S.L.P 1253 Dodoma.

Simu +255 26 2320156

Barua pepe: info.dodoma@tmda.go.tz

Kanda ya Kusini

Jengo la PSSSF,

S.L.P 1447, Mtwara.

Simu: +255 232334655

Barua pepe: info.mtwara@tmda.go.tz

Kanda ya Magharibi

Jengo la TUWASA,

S.L.P 520, Tabora

Simu +255 262606082

Barua pepe: info.tabora@tmda.go.tz

MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA



Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

UDHIBITI WA MATANGAZO YA BIDHAA

